Orodha ya Hati Zinazohitajika ili Kutuma Ombi la UNM Care au Out-of-County

Tunakuomba uwasilishe **hati fulani za uthibitisho** pamoja na ombi lako la UNM au Out-of-County Care. Tunafanya hivyo kwa sababu tunahitaji kuthibitisha –

- Wewe ni nani (utambulisho)
- Mahali unakoishi (anwani)
- Kiasi cha pesa unazopata (mapato)
- Kiasi cha pesa ulizo nazo katika akaunti zako za benki na za uwekezaji (mali)

Kitengo cha Usaidizi wa Kifedha cha UNM Hospital kitapitia ombi lako na hati za uthibitisho na kukujulisha ikiwa wanahitaji hati nyingine zozote kutoka kwako.

Hapa chini kuna orodha ya hati tutakazokubali. Lakini ikiwa huna hati zilizoorodheshwa hapa, tujulishe. Tutashirikiana nawe kutafuta suluhisho.

Wewe ni Nani (Utambulisho)

Tutakuomba 1 kati ya hati hizi kwa **kila mtu katika kaya yako**. Hati hizi hutusaidia kuthibitisha utambulisho wako na utambulisho wa kila mtu anayeishi nawe. Tutakubali yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa chini (nakala pekee tafadhali).

- Pasipoti (ya kigeni au ya Marekani)
- Cheti cha kuzaliwa (cha kigeni au cha Marekani)
- Kitambulisho cha picha (leseni ya dereva, kitambulisho kilichotolewa na serikali, kitambulisho cha kazi au cha shule)
- Kadi ya mpango wa Social Security
- Cheti cha Mzaliwa wa Kihindi
- Hati za talaka
- Rekodi za shule au rekodi za kituo cha kutunza watoto mchana
- Rekodi nyingine za serikali, kama vile viza (viza ambazo muda wake wa kutumika umeisha zinakubaliwa)
- Taarifa kutoka kwa mhudumu wa kesi, mhudumu wa afya ya jamii, mtoa huduma wa afya au shirika la jamii linalokujua wewe na hali yako

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

Ikiwa huna yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapo juu, tujulishe. Tutashirikiana nawe kutafuta hati nyingine ili kutimiza sharti la uthibitisho wa utambulisho. Kumbuka, **huhitaji** kuwa na uraia wa Marekani au kuwa na hali fulani ya uhamiaji ili kutimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care.

Mahali Unakoishi (Anwani)

Tutakuomba hati iliyo na jina na anwani yako. Ikiwa unaomba UNM Care, inapaswa kuonyesha kwamba unaishi katika Kaunti ya Bernalillo au Kaunti ya Sandoval. Ikiwa unaomba Out-of-County Care, inapaswa kuonyesha kwamba unaishi katika kaunti nyingine ya New Mexico (si Bernalillo au Sandoval). **Unahitaji hati moja tu kati ya hati hizi kwa kaya nzima.** Tutakubali yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa chini (nakala pekee tafadhali).

- Waraka wa mshahara
- Bima ya gari
- Bili ya huduma ya nyumbani (umeme, gesi, maji, simu, intaneti)
- Mkataba wa kupangisha nyumba, hati ya rehani au hati ya ushuru wa jengo
- Bili au taarifa nyingine
- Uthibitisho wa kujiandikisha au kumwandikisha mtoto katika taasisi ya elimu
- Fomu za malipo ya kodi ya mapato
- Hati ya malipo ya Social Security, malipo ya ulemavu, malipo ya uzeeni au malipo ya kustaafu
- Taarifa kutoka kwa mhudumu wa kesi, mhudumu wa afya ya jamii, mtoa huduma wa afya au shirika la jamii linalokujua na linalojua hali yako

Picha imetolewa katika www.pnm.com/definitions

Ikiwa huna yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapo juu, tujulishe. Huenda tukaweza kushirikiana nawe ili kukubali hati tofauti.

Kiasi cha Pesa Unazopata (Mapato)

Tutakuomba hati zinazoonyesha kiasi cha pesa ambacho wewe na kila mtu katika kaya yako hupata kwa mwezi. Tutakubali yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa chini (nakala pekee tafadhali).

- Nyaraka za mshahara
- Fomu za malipo ya kodi ya mapato
- Barua kutoka kwa mwajiri inayotaja mapato yako ya kila mwezi
- Hati za kuweka pesa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki

This translation was completed by LanguageLine Solutions.
Swahili

- Barua au nakala za hundi kutoka kwa mipango ya Social Security, Worker's Compensation, Veterans Affairs au Bureau of Indian Affairs
- Rekodi za kumbukumbu za ajira ya binafsi
- Taarifa kutoka kwa mhudumu wa kesi, mhudumu wa afya ya jamii, mtoa huduma wa afya au shirika la jamii linalokujua na linalojua hali yako

Ikiwa huna makazi, umefilisika au unapokea msaada wa SNAP, TANF au WIC, huhitaji kuwasilisha hati za uthibitisho wa mapato.

Ikiwa huwezi kuthibitisha mapato yako au hupati mapato, unaweza kuandika taarifa inayosema hivyo. Taarifa yako inapaswa kueleza jinsi unavyolipa gharama za kila siku kama vile chakula, nyumba na usafiri.

Ikiwa mtu unayemjua hukusaidia kifedha, mtu huyo atahitajika kuandika Barua ya Usaidizi. Katika barua yake, anapaswa kueleza anavyokusaidia, anacholipia, kiasi anacholipa na huwa anafanya hivyo mara ngapi. Hakikisha kwamba wewe na mtu anayekusaidia mnatia sahihi barua hiyo na uiwasilishe pamoja na hati zingine.

Unaweza pia kujaza Fomu ya Taarifa ya Mapato (Income Declaration Form) inayopatikana katika tovuti yetu.

Kiasi Ulicho Nacho Katika Akaunti Zako za Benki na Uwekezaji (Mali)

Ili kutimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care, huwezi kuwa na zaidi ya jumla ya $20,000 kwenye akaunti zako za benki (za kawaida na za kuweka akiba) na akaunti za uwekezaji. Hatutakuomba uchukue pesa kutoka hazina yako ya kustaafu, dhamana, akaunti za kuhifadhi pesa bila kuzichukua kwa kipindi maalum (certificates of deposits, CD) ili kulipia bili zako za matibabu. Hata hivyo, ikiwa tayari umepokea pesa kutoka kwake katika mwaka huo au ikiwa fedha hizo zilifikia kipindi cha kutolewa katika mwaka huo (hii inamaanisha kuwa tarehe imefika ambapo lazima ulipwe kwa uwekezaji wako), fedha hizo zitahesabiwa kama mapato.

Tutakubali taarifa za akaunti za hivi karibuni za akaunti zozote za kawaida, za akiba na za uwekezaji ulizo nazo (nakala pekee tafadhali).

Kumbuka – Nyumba yako, gari na hazina ya kustaafu havijumuishwi. Huhitaji kuwasilisha hati zozote kuhusu mali hizo.

Je, itakuwaje ikiwa sina hati za uthibitisho?

Ikiwa huna hati hizi za uthibitisho, tafadhali tuambie! Tuko tayari kushirikiana nawe kutafuta suluhisho.

Mpango wa UNM Care au Out-of-County Care unaweza kuidhinisha hati nyingine ambazo hazijaorodheshwa hapa.

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

Je, itakuwaje ikiwa nina maswali au ninahitaji usaidizi?

Tutembelee –
Main Financial Assistance Office
1131 University Blvd, Suite D
Albuquerque, NM 87102

Tupigie simu – 505 272-2521

Nenda kwenye tovuti yetu –
Kwa taarifa zaidi, Sera yetu kamili ya Usaidizi wa Kifedha na tafsiri za hati hizi, tafadhali nenda kwenye tovuti yetu –
https://unmhealth.org/patients-visitors/billing-insurance/

Unaweza pia kutazama ombi la UNM Care na Out-of-County Care hapa. Lakini unahitaji kupanga miadi ili kutuma ombi la mpango wowote kati ya mipango hiyo miwili. Tafadhali piga simu kwa 505 272-2521 ili kupanga miadi yako na Mwakilishi wa Huduma za Kifedha.